At the same time, ninaona, the retirees in our country here, wanapata shida sana, kwa sababu sijui ni Act ya Parliament au ni Act ya wapi ambaye haihusishwi kuona ati mtu akipewa barua ya retirement benefit zake zote ziwe zimetayarishwa. Kwa sababu unaona ni wazee wengi na nikisema hivyo ninasema wazee, akina baba na akina mama, wengi hufa, kabla hawajapata

benefits zao. Nairobi iko hapa, Treasury, iko hapa, inakua mtu anaenda, anuaza ng'ombe ili apate tikiti ya kupata hizo pesa, na mwishowe anachoka, kwa hivyo mimi ningependelea, hapa tuna ma-ofisi ya Treasury, kwa mikoa, kama ingekua bora, kama pensioners wangekua baada ya kupata barua ya retirement, benefits zake zote zinatengenezwa, anazipata kwa Treasury ile iko karibu naye. Kwa mfano kama hapa Nakuru sasa, kama ingekua inasafirishwa na kuletwa kwa Treasury ya Nakuru, watu wangekua wakipata hapa karibu, lakini habari ya kwenda Nairobi saa yote, inachokesha, wengine ni wazee, wanashindwa.

Kwa hivyo, mimi ninaonelea ni pesa nyingi sana ya wananchi wa Kenya, ya wastaafu, ambayo hupotea kwa serikali. Na sijui mwishowe hiyo pesa huenda na nani, kwa sababu nikiweza kufuata na nishindwe, halafu mimi ninasema hathuru niwachane naye, sijui hiyo pesa mwishowe huenda wapi? Kwa sababu nimeonelea hata wacha wale ambao wamestafu, nimeona ma-ofisa wengine wa serikali wakiaga, wajane, wanajaribu kufuata hizi fedha, hakuna mtu wa kuwasaidia, kwa hivyo ningepomba serikali iwe na roho ya huruma na kujaribu kusaidia, kama ni hawa wajane, benefits za ma bwana zao waweze kupatiwa kwa urahisi either through the DC's office au the Chief's office.

Neno la mwisho ambalo ningependa kusema ni...

Com. Salome Muigai: Na una nusu dakika ya kuulizwa.

Phanuel M. Muraya: Okay, asante sana, hii ni habari ya hii government properties, siku hizi tunaona, zamani ku-condemn a building ya serikali ilikua ina-formiwa a board of survey. Lakini siku hizi hata gari unaona kama ni gari mpya, zinafanyiwa survey ya board ya kienyeji hivi, unaona gari ya serikali inaenda na mtu. Shamba unaona inaenda na mtu. Go to Nairobi, kama legal area, pahali yote Ministers used to stay, unakuta hiyo land yote ni kama imepewa watu. Sioni ni haja gani ama ni maana gani government property iwe ikipewa watu individuals. Na ni hayo ningependa kusema, asanteni sana.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa maoni yako, Bwana Phanuel. Sasa namwita Councillor G.M. Ndegwa?

G.M. Ndegwa: Thank you Commissioners, my names are Councillor Geoffrey Mutahi Ndegwa. Mimi ni nominated Councillor from Nakuru County Council. Nimewajibika kutoa maoni ya kibinafsi kwa sababu nashiriki kutoa ile ya Council na chama pia. The following are my opinions.

Kitu cha kwanza ni ya kwamba mimi ninaunga mkono serikali ya unitary government. Therefore I don't need to say about presidential powers sababu hile ina Prime Minister na wengine na pia kama vile ilivyo isiwe ni ya political parties, iwe ni ya watu ambao ni wa Kenya.

Jambo la pili haya mambo yote ambayo tunalalamika hapa, yako kwa sababu ya lack of good management. Sijui tutahitaji Katiba iweze kueleze kwamba President yeyote ama government officer ambaye atakuwako, asiwe bad manager, for instance, tukienda kupanda mti hapa juu, PC anakuja na ma-ofisa wote wa serikali na magari yote. That is wastage of human resources, instead of empowering the Forester and the local community, wanatumia pesa hizo zote na magari makubwa kuja kupanda miti

miwili. If you compare the value of two trees na ile kazi yote wamekuja, ni waste of resources.

Wakati President ako na function, Ministers na sisi ma diwani tunafunga ofisi kwenda kumlaki, the Constitution should be very clear on the duties of the President. Sio tu kwenda kutumia resources, kununua jet yake ya ajabu, mambo mengine, mlolongo wa magari, awe kama President Nelson Mandela, ambaye hata kwa hospitali anaenda bila bodyguard. We want to minimize the security details of all government officer, not the President alone.

Three, madam Chairman, ni mambo ya food security. We would like the Constitution not to leave the role of food security to the Minister for Agriculture. Katiba ieleze kwa sababu nchi hii ni ya kilimo, wamama wamelia mambo ya maziwa na nini, Katiba ii-entail ya kwamba, it is the role of any government to make sure that it's citizens have sufficient food. Hiyo ni mambo ya kuwaeleza ya kwamba, mambo ya marketing iondolewe kwa serikali, cereal boards iwe scrapped, KCC iwe scrapped. The local communities wapewe uwezo wote.

When we go to the Local government, I am a Councillor lakini the current system of the local government is not clear. The Minister for Local government is the only Minister who has a budget of more than 4 billion ambayo inatumika headquarter peke yake. The Minister for agriculture has officers at the division, district na province. Lakini Minister wa local government, sisi ndio tunampelekea pesa. We would like it to be a local assembly, not a Minister for a Local government trying to overrule the decision.

Ma diwani wawe wakichaguliwa hivyo na pia ma Mayor na Chairmen, mimi naungana na wengine, wawe wachaguliwe direct. Na kuwe na community opinion poll. Wananchi wenyewe wawe na poll ambayo watakua wakipiga baada ya miaka miwili, kuwa –access mambo ambayo wanataka. Lakini, when we de-link development kutoka kwa siasa, Katiba iweze kutengeneza development kutoka kwa siasa. Mjumbe asionekane yeye ndio analeta maendeleo, Councillor asionekane yeye ndio analeta maendeleo, maendeleo yaachiwe wenyewe, waamue mimi ni mwakilishi wao. Mimi sio mshirikishi wa maendeleo, hivi ya kwamba wakiamua wanatengeneza barabara, wananalika mimi ni mheshimiwa ndio, lakini wanaamua na tunashirikiana nao kutafuta pesa na kuingia katika ma-ofisi.

Before I finish nataka kusema ya kwamba mambo ya DDC, the Constitution should be clear on rural development. Madam, Chairman, utaona ya kwamba, currently most of us including you, tumelewa na taabu nyingi sana na wamama ambao hawajakua na masomo na mambo mengi. But immediately after school, tunaenda Nairobi, maendeleo yote tunafanyia huko. Although this country is a capitalism government, maendeleo yaweze kufanywa kwa rural development. Sisi ndio tunatoa maji hapa, lakini watu wa Municipalities wanakunywa maji. Sasumwa dam iko Nyandarua, lakini watu wa City Council ndio wanakunywa maji na ule mwananchi wa Sasumwa hata hajui maji yanatoka kwakwe. That means the resources of the community should be shared na ziwe beneficial kwa wao. Before my time expires, I am calling for a private police force. The establishment of a private police like in other countries. This madam Chairman, ni kwamba, wakati ajali imetoka, Kenya Police

ndio wanaenda kuchunguza ajali hiyo. Na hata wakikuta mwenye makosa yuko pale kwa vile corruption iko sana, wanaandika report ambayo ni true ambayo itaenda kotini na huyu mwananchi wa kawaida hawezi ku-challenge hiyo decision ya police. So we are calling for a private police kama vile tuliona detective from Ireland, wale akiina Troon na wengine, from Scotland sorry, na wengine. We want to have a private police, CIA, FBI, hivyo.

Hivi ni kwamba, juzi kumekua na mauwaji mengi sana Nairobi, watu wanauawa mysteriously. Balistic experts wakija wanatoa repoti yao ni hiyo ndio kikomo. No more investigations, wewe unaenda ku-hire wakili, anakuitisha a hundred thousand, mwananchi wa kawaida hana lakini kama kungekua na private police, you could hire your private investigators. We also have an example,

Com. Salome Muigai: The last point Bwana Diwani, nimekipa dakika saba tayari.

G.M. Ndegwa: Thank you. Kwa mfano, wakati ambayo umesikia wengi wakitaja hapa mambo ya clashes, nobody could take his/her prosecution to other sources, other than the advocates, therefore, kukiwa na private prosecutors wataweza ku-file on behalf of the poor man. Finally, ili nisipoteze wakati wako, ni ya kwamba, the civil service should be de-linked from politics.

An example is that the current Secretary State of America, Collin Powell was appointed during Ronald Reagan terms, ame-serve serikali ya Bush, ame-serve serikali ya Clinton, ame-serve serikali hii ambayo iko. What I am saying here Madam, ni ya kwamba, civil servant, awe ni civil servant aendelee hivo hivyo. And finally nisipoteze wakati wako, the tenure of government officers.

Com. Salome Muigai: Bwana Diwani unajua mimi ni mgeni wako, sitaki kukua mgeni mbaya lakini usinishurutishe kuwa mgeni mbaya kwa kukuambia saa imeisha.

G.M. Ndegwa: Ningekua nimemaliza, ya kwamba the tenure of government officers itengenezwe katika Katiba kwa mfano, nyinyi mkimaliza kazi ya Commission, mtakua watu ambao tutakuna huko nje, lakini tungetaka ile heshima kama vile mtu mmoja ameongea kuhusu retired officers, the dignity of retired citizens ambao wamesaidia kufikisha hapo, kama British war veterans wamekua wakiheshimiwa, wawe wakiheshimiwa, hata diwani akiacha kazi, awe akiheshimiwa, hata judge akiacha kazi, awe akiheshimiwa, Katiba ianze mpango huo. Asante sana.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Diwani, ujiandikishe, kuna swali kwa diwani? Hamna, basi jiandikishe. Sasa ninamwita Ann Nduta Njoroge? Yuko.

Ann N. Njoroge: Majina yangu ni Ann Ndunta Njoroge kutoka Tabuga. Ninakuja tu kusema maneno mawili, inanihusu kwanza na inahusu kila mmoja. Sisi kama wa mama wengine ni wakulima mahindi na maziwa, hata mboga. Na ukishaweka bidii, mazao inakua hakuna mahali ya kuuza. Na tena tunasomesha watoto kwa jasho. Watoto wetu wanakosa kazi. Watoto tunaona sio wabaya, maana watoto wengi wanafanya uhalifu shauri ya kukosa kazi, sasa tunauliza tufanye nini? Serikali itukumbuke sana kama sisi wazazi, kutafutia watoto wetu kazi, tena upande wa hospitali, ndio ulikuwa wa usaidizi wowote kwa

raia wa kawaida, sasa sisi tunakufa kinyumbani, hana pesa ya kwenda hospitali hata ya kununu card. Ukiandikiwa dawa, hakuna pesa ya kununua, sasa tunategemea nani. Sisi tunategemea serikali itusaidie.

Com. Salome Muigai: Unapendekeza serikali ifanye nini mama?

Ann N. Njoroge: Tunapendekeza upande wa serikali

Com. Salome Muigai: Ufanye nini?

Ann N. Njoroge: Irudishe kama kawaida ya zamani.

Com. Salome Muigai: Kawaida ya zamani ilikua nini?

Ann. N. Njoroge: Ilikuwa kama sisi tunaenda kama medical, tunatibiwa vizuri na tunasaidika lakini sasa hata medical, hata hospitali ya watu kawaida ni sawa sawa tu. Tena tunalima viazi na hakuna mahali ya kupitia gari. Tena tuangaliliwe sana upande wa barabara.

Com. Salome Muigai: Asante sana mama, jiandikishe pale. George Gethi?

George Gethi: Thank you madam Commissioner. My name is George Gethi. I wish to propose that after this Constitution is prepared and some document approved, we should have a mechanism whereby Parliament or any other individual who comes in higher authority will not be in a position to compromise anything and that the document should only be amended after a referendum from the people who would have struggled so much to have it spared. I also submit that any Member of Parliament, who fails to perform or deliver, there should be a mechanism in the Constitution empowering the constituents, to get read of him and replace him with a more productive material in Parliament than he is.

The third point that I would like to submit is that I would like the Provincial administration, all the way from the Chief to the Provincial Commissioner be completely scrapped and its place we get people elected by the people, the Chief be elected by the people, the Commissioner gets elected by the people and even the Provincial Commissioner gets elected if ever the authority feels that, that position should be existing.

The fourth point is that the Local authority have always been a burden to society, in that they have not been delivering and I would submit that the local authority should be made autonomuous to an extent whereby they would be making their local decisions on matters of development and progress, within themselves and they would have that capacity to make those decisions. With those few points, thank you very much, madam Commissioner.

Com. Salome Muigai: Tuna maswali mawili kwako, subiri tafadhali.

Com. Ratanya: Mr. George Gethi, the first question is about the amendment of the Constitution. You have recommended

just one method or procedure of amending the Constitution, that is by referendum. Is that the only proposal you have or you have another one?

George Gethi: I only have that one for the time being, referendum, that is consulting the community.

Com. Ratanya: Okay, now the other question is about Provincial Administration, you are saying that Provincial Administration should be scrapped and yet you are also saying the same officers should be elected, that we elect the DC, PC down to the assistant chief, are you replacing the appointment or the method of appointment maybe this time they are appointed by the government, or you are suggesting now they should be elected instead of being appointed, or you are scrapping the whole system? Because the whole system because it is not very clear.

George Gethi: I am for the retention of the present system but elected not appointed because when it comes to the delivery of service, an elected person delivers differently from a person who is answerable to only one person somewhere else. Whoever is elected will be answerable to whoever elected and would have come from the masses. Not from one individual saying that Kamau Njoroge is the PC tomorrow, this is what I mean.

Com. Ratanya: So you want the system to continue, Provincial administration but with elected officials?

George Gethi: Yes.

Com. Ratanya: Okay.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Gethi, swali langu ni kuhusu hiyo yenye umetueleza ya kuwa watu wamechaguliwa, sisi tumesikia malalamishi mengi pale tunaenda kuwa madiwani wetu wenye tumechagua ndio wenye kuchukua ma-plot zetu, ndio wenye kuziua, ndio wenye watu wametuambia tufikirie Katiba inaweza kufanya nini juu yao, tumesikia pia malalamishi mengi kutoka kwa wanabunge, baada ya kuenda kutetea watu, wanaenda kujiuongeza mishahara. Sasa inaonekana kama kuwa tu mtu amechaguliwa sio lazima afanye lile tulimchagulia. Wewe unaona uchaguzi tu, tukishamchagua imetosha ama kuna mambo mengine yenye ingeongzwa ili kuwawezesha watu wenye wamepatiwa jukumu na wananchi kuwapa ile matakwa ya wananchi?

George Gethi: Kwanza madam Commissioner, that entirely on Electoral Commission, the way the electoral Commission is absolutely un-desirable because of them get, they are not actually elected as it were. Many of them do not do their work properly. They are not entrenched as it were. Like in the Security that goes with elections, you find that people get elected due to certain forces, forcing issues through insecurity, creating instability during elections. So that you get the wrong people in the right places. So that the masses do not get the right materials which they would want to have, through electoral Commission's failure.

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Gethi kwa maoni yako. Tafadhali jilandikishe pale. Margaret Wairuri?

Tungetaka mtu mwenye angetufanyia tafsiri tafadhali.

Margaret Wairuri: Ndirenda kuuga atiriri.

Com. Salome Muigai: Aanza na jina lako?

Margaret Wairuri: Njitagwo Margaret Wairuri.

Translator: Anasema anaitwa Margaret Wairuri.

Margaret Wairuri: Ndirenda kuuga niwega muno niundu wa guka gutuuria thina wiitu.

Translator: Anasema ni asante kwa kuja kutuuliza shida zetu.

Margaret Wairuri: Thina witu tukoragwo twina muingi muno tugakira.

Translator: Anasema kwamba shida zetu ni nyingi lakini sisi hunyamaza.

Margaret Wairuri: Tukaga uria tungira.

Translator: Tunakosa mtu wa kumwambia.

Margaret Wairuri: Mbere ni kuaga guaguthiira.

Translator: Kwanza, njia ya kupitia,

Margaret Wairuri: Wa keru, tugathomithia ciana na mabuti.

Translator: Pili, tunawapeleka watoto wetu shuleni kwa njia ya kulima mabuti.

Margaret Wairuri: Mundu ari na ciana inya ithatu mucii.

Translator: Mtu ako na watoto wane au watatu nyumbani.

Margaret Wairuri: Na nituthuranaga.

Translator: Sisi hufanya uchaguzi.

Margaret Wairuri: Na riu nimurenda tumuhe miti.

Translator: Wengi wetu wanapenda tuwape kura.

Margaret Wairuri: Na riu ciana icio ri. Ona mutituandikagira o nomwe.

Na gutiri maregete.

Translator: Anasema kwamba hatupati nafasi ya kuandika hawa vijana kazi au wasichana hata kama ni kazi ya kuosha vyoo.

Margaret Wairuri: Na tumuthuraga mugatuaririe.

Translator: Tunawachagua ili muweze kutetea haki zetu.

Margaret Wairuri: Na ciana ciitu irio micii. Ona nikiu taabu muno iri miingi micii na wuici ukaingiha.

Translator: Nasema ndiposa watoto wengi wako nyumbani, shida nyingi na uizi unakuwa mkubwa.

Margaret Wairuri: Tondu gutiri mwana ungigurira gakuo.

Translator: Maana hakuna hata mtoto mmoja anaweza kujinunulia nguo.

Margaret Wairuri: Na riu ri, niwega. Ningi iria tene ni kurakiri dairy. Niratwaragwo.

Translator: Ni vizuri hivyo, lakini zamani tulikua na dairy ambazo zilikua zikinunua maziwa yetu.

Margaret Wairuri: Riu nikunyuo rinyuagwo ta mai.

Translator: Na hivi sasa tunanywa maziwa haya kama maji.

Margaret Wairuri: Tukarima mbembe.

Translator: Tunalima mahindi,

Margaret Wairuri: Niguthecwo ithecagirwo micii.

Translator: Inaharibikia kule galani kwa kudungwa na wale wadudu.

Margaret Wairuri: Tondu mundu ndakiri na ciana cia gukiria.

Translator: Maana hauna watoto wa kula yale mahindi.

Margaret Wairuri: Na ningiri ni wega. Nimweka wega muno niundu wa guka gutucerera guturia thina witu. Na riu uguo ri, mbembe kurima ikunia ukendia magana mana ri, matatu ri, tukarima waru ri. Urimage ukeendia magana meri, ikunia. Ona angikorwo urimite acres ciganari, nduri kindu ungiiona.

Translator: Nasema ni asante kwa kuja kwenu kujua shida zetu, jambo ambalo ni kubwa ni kwamba tunakuza mahindi, maharagwe na hata kila kitu, lakini shida ni kwamba ukiuza gunia ya mahindi, unauza mia mbili ama mia nne. Hata ukiwa na shamba hekari moja, uyauza yale mahindi hakuna kitu utajifanyia.

Margaret Wairuri: Na ningi kura nitukumuhe no mumenye twamutuma wira.

Translator: Anasema kura tutawapa lakini tumewatuma kazi.

Margaret Wairuri: Mugatwariririe.

Translator: Muende mukaongee.

Margaret Wairuri: Ciana muturutire mucii na ona guciandikithia, na madereva magathii magathomera, gutiri. Akerwo athii mucii, eterere mieri itatu.

Translator: Anasema kwamba vijana wameenda kusomea uu –driver lakini wanaambiwa wagonjee nyumbani miezi tatu, uje kazi.

Margaret Wairuri: Akarega kuona marua gwitwo.

Translator: Miezi mitatu inaishi hakuna barua.

Margaret Wairuri: Ta gitare wina ihii inya ithano.

Translator: Ukihesabu ukiwa na vijana wane watano.

Margaret Wairuri: Na airitu marioho.

Translator: Wasichana bado wako pale.

Margaret Wairuri: Na hatiri mundu uri wira.

Translator: Na hakuna hata mmoja aliyo na kazi.

Margaret Wairuri: Mugithiaga gutuariria ki?

Translator: Tunaenda kuongea kuhusu nini?

Margaret Wairimu: Ndiri na maingi.

Translator: Sina mengi,

Margaret Wairimu: No macio ngwendaga kumuiru.

Translator: Ni hayo tu asanteni.

Com. Salome Muigai: Mama ningetaka kukujulisha kuwa hii ni Tume ya Katiba na sio yenye watu wenye huja kuchukua kura, hatuja chaguliwa na kura, na wajumbe, na madiwani ndio wanafanya kazi yenye umesema, lakini pia sisi tumekusikia.

Tume imekusikia na shida zako.

Margaret Wairuri: Ti mumatuarire mathina macio. Acio marena.

Com. Salome Muigai: Wanatakiwa kuwa hapa wakusikize moja kwa moja. Lakini Councillors, wako, ma diwani wako na wataeleze mjumbe vile ulisema. Asante sana jiandikishe pale. Kiama Wachira?

Kiama Wachira: Kwa jina ninaitwa Kiama Wachira. Na mimi ni mkaaji wa hapa. Mimi sina mambo mengi ya kuzungumza ama ya kuuliza ama ninayo. Isipokua mimi ninasikia mna-harass watu ati dakika saba, kumi na hiyo ni makosa moja mumekuja kufanya, maana watu wana mambo mengi, na hayawezi kumalizwa na dakika kumi na tano, ama dakika tano. Kitu kimoja, sasa ni anze na mambo yale yamenileta hapa.

Ya kwanza, ni kwamba Katiba iliyo sasa, inayofanya kazi, inamatope ya kibeberu, hiyo inatakiwa badala ya kusema irekebishwe, parts, hapana, itupiliwe mbali yote, watu wetu wamesoma sana, na wana ujuzi mwingi, watengeneze Katiba ambayo ni ya kiafrica, wanajua tabia zetu, wanajua taabu na hiyo Katiba inayofanya kazi ni ya kibeberu. Iondolewe na mambo yake yote yawe demolished, tutengenezewe Katiba ya kufaa sisi na taabu zetu na utajiri wetu. Hiyo haina faida.

Jambo la pili, katika Kenya, mambo ya corruption yamepata mizizi mikubwa hivi kwamba, kuiondoa ni shida isipokua tubadilishe na pawe na serikali iliyo na nguvu sio serikali weak kama iliyo sasa. Serikali ambayo, inauwezo ya kuiondoa corruption kwa ma korti, ardhi house, police, kwingineko kote kunahusikana na mambo ya public. Corruption iondolewe. Chief, yeye ndiyo base ya Office of the President. I want chiefs, ma chief wetu ndio chanzo cha corruption. Wawe wakichaguliwa na watu wenyewe, lakini mshahara wachukue kwa serikali. Na akikataa kufanya vile watu wanavyopenda, wapewe haki ya kumuiondoa na kuchagua mwingine. Sababu wao wameshindwa na kazi zao, wameshindwa na kuiondoa pombe haramu, wameshindwa na kuiondoa unywaji wa changaa na uvutaji wa bangi na kadhalika, hiyo imekua ni biashara kwao, na raia wanaumia.

Ingingine, ni hili jambo mnasikia ya kwamba watu wanalalamika ya watu wanaofanya makosa katika serikali na kua-abuse, kutusi mamlaka walio nayo kazini. Ikiwa mtu amefanya kosa lolote katika mahali anapofanya kazi, akiwa ni mfanyikazi wa serikali, asiwe transferred at all, afutwe kazi. Sababu makosa aliyonayo hapa, imemukolea ndani ya mafupa. Na akienda mahali fulani, ati ni transfer anakwenda kuongeza hiyo mambo na tena kufundisha wetu wengine mambo ya corruption na mambo mabaya. Afutwe na sheria ikiweza kumfunga imfungue. Jambo lingine ni watu hao wanaofanya kazi ya kua-abuse offices. Akiiba pesa ya serikali ama raia, mtu huyo kabisa afanyiwe uchungusi akionekana amefanya hivyo, si kifungo peke yake ama transfer, afungwe na tena hiyo mali alipe, asikubaliwe kwenda nayo bure. Sababu watu wetu wanajua ya kwamba hata kama ukifutwa kazi, na pesa umeiba, unakwenda kuwa tajiri. Hapana, walazimishwe kurudisha. That be a must, warudishe.

Com. Salome Muigai: And you have a half a minute to finish up.

Kiama Wachira: I beg your pardon?

Com. Salome Muigai: You have actually gone through your time of five minutes, I am giving you another half a minute to wind up.

Kiama Wachira: That is why I told you that you came to joke. You didn't come to hear our complaints, you came hear to joke. Hakuna mtu anaweza kumaliza maneno yake kwa dakika tano, ni mtu wa aina gani huyo. Ana mambo ya aina gani.

Com. Salome Muigai: Sasa ile nusu dakika yenye nimekupa, umeitumia kuniambia hivyo basi...

Kiama Wachira: Sio neno, hata ukunifukuza, nitakwenda tu.

Com. Salome Muigai: Sikufukuzi lakini saa imekwisha.

Kiama Wachira: Tafadhali ningepuliza hata serikali yote, iwape muda msikize sisi, tuna-complain very strongly na nyingi ambazo tunaumizwa na serikali yenyewe, na watu wote, badala ya kupewa muda wa kujisungumza, mnatuambia dakika tano, haifai. Okay sawasawa Asante.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mzee. Na sasa nintaka kurudisha mswada wa time mwenye ukumbi. Tumekua tukichukua dakika tano na kila mtu analalamika hazitoshi na ninakubaliana nao, lakini sasa tumefikia saa nane na dakika ishirini tatu, inaelekea saa nane na nusu, bado ninawatu karibu thelathini wenye wangetaka kuzungumza. Sasa tuna mambo mawili, tuweke vile dakika tano tano, na nusu ya hao watu watazungumza kabla hatujafunga, amatuzikatie ziwe dakika tatu, na watu wengi wapate nafasi ya kuzungumza?

Sisi akina mama tunafanya hizi decisions kila siku, umepika chakula, wageni wanaingia, unaanza kukata ration kidogo kidogo ndio kila mtu apate kidogo, kwa hivyo tafadhali tungekata hizi time, ziwe dakika tatu, ueleze sana sana ile mambo yenye hujasikia mwingine akizungumza. Kwani ukienda nayo nyumbani, tutaenda kutoka Subukia na tumewacha hiyo maneno, kwa hivyo ningetaka uanze na ile haijzungumzwa na mtu kwa dakika zako tatu, halafu ukikua bado una dakika nyingine moja, utaeleze ile ya kurudia. Tunaelewana, na sasa mtu wa kwanza, mwana tume mwenzangu ana jambo la kusema.

Com. Raiji: Unajua hii mambo ya saa kama wale ambao wanakuja kuchangia, wangetueleza yale mapendekezo ya yale maneno wangetaka tuingize kwa Katiba, hata dakika hizo tano zitakua mingi. Lakini wengi wenu sana wanakuja kuzungumza story ndefu, badala ya kulenga pointi yenyewe. Kwa hivyo kama Chairperson amesema dakika tatu, tafadhali mjaribu kulenga pointi yenyewe. Give your specific recommendations on the proposals ya yale mgetaka tuingize kwa Katiba. Kwa sababu hiyo ndio imetuleta hapa, ukisema tungetaka kuingiza A,B,C,D, hata hiyo dakika tatu itakua nyingi. Asante, Chairperson.

Com. Salome Muigai: Mwanatume mwenzangu ni wakili. Lenga hapo na umalize, mimi ni mwalimu ninasikiza story. Lakini ile yenye tungetaka kufanya ni vile tunatumia muda. Aanza na yenye haijasikika, tuambie mapendekezo yako, halafu ukiwa na time, utueleze hayo mengine. Na mtu wa kwanza kuzungumzia hii time frame mpya ni Constance Njoroge? Ah Constance

Njoroge ulizungumza jana, kwa hivyo kabla sijakupa hiyo nafasi, nitampa mtu mwingine, pole, wale watu wenye walizungumza jana ndio nitamalizia malizia nao, ndio tusikose mtu mwenye hakupata nafasi jana. Okay. Ninaelewa lakini bado nilikupa nafasi jana, nitakupa wakati mwingine, lakini ni baada ya wale wengine kupata nafasi ya kwanza. Eliud Kimani?

Eliud Kimani: Kwa majina ninaitwa Eliud Kimani, na nina kaa hapa Umoja. Ni mkaaji wa Ndondori location. Mapendekezo yangu ni kidogo tu sio mengi, kwa sababu kuna mambo ambayo tunaona County Council wanatufinya nayo, katika mahali tumejenga ma plot, halafu na wao wanakuja kuchukua kodi katika zile plot zetu. Kwa hivyo katika ile kuchukua pesa hizo, tunaonelea wanatufinya kwa vile hawakutusaidia kujenga hizo plot. Plot tulinunua wenyewe na baada ya kununua plot wenyewe, tulijenga wenyewe, tumejenga wenyewe, halafu baadaye wanakuja kuchukua rent ama licence kutokana zile building zetu. Kwa hivyo pendekezo langu, ningeliza kama watachukua hizo pesa, either tugawane nao ama watuwachie hizo pesa badala ya kufanya hivo, wachukue kutoka kwa centers zao.

Jambo la pili, ni kuhusu habari ya watoto wetu. Watoto wetu ambao tunawazaa na tunawasomesha, ningeliza Katiba itusaidie serikali iwe ikiwachukua na kuwatafutia ama kuchukua jukumu la watoto hawa. Kwa sababu sisi kama watoto tunashindwa na kuwahangaikia ili wapate matumishi yao ama maisha yao. Kwa hivyo ningependekeza, Katiba isaidie wazazi kuwasaidia watoto wasaidiwe na serikali kutoka wanapomaliza masomo.

Jambo lingine ni kwamba, mimi ni mzee ambaye nime-retire. Na vile nime-retire ningeliza Katiba inisaidie wakati watu wengine wanapo ongezwa pesa ya pension na mimi niwe nikiongezwa. Ama mwananchi wa kawaida ambaye ame-retire awe akiongezwa pesa pamoja na wale wengine.

Jambo lingine ni kwamba upande wa shule, kuna sheria ilipitishwa ya kwamba watoto wasipigwe. Mimi ningependekeza, hiyo sheria inatuharibia watoto, kwa sababu watoto wetu inaonekana wasipopewa discipline ama kufundishwa vizuri na kupigwa kiboko moja, wanakua wabaya zaidi kwa sababu hawapigwi. Kwa hivyo ningeliza Katiba ikitengenezwa, iangalie sana upande huo wa kupea mtoto discipline.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa kuweka dakika zako tatu. Jiandikishe pale tafadhali. John Kagiri? Amos Ngugi Njoroge? William Mwangi? Ni mwanafunzi, mzee huyo hatakua ni wewe, Joseph Kariuki Maina? Una dakika tatu Kariuki.

Joseph K. Maina: Yes Madam. Kwa majina yangu yote ni Joseph Kariuki Maina. Ile kitu ningependa kuongea ni kuhusu idadi kamili ya umiliki wa ardhi.

- Mtu asiwe na zaidi ya hekari elfu moja.
- Pili, mbunge awe ameo au ameolewa naa hata Rais na Councillors pia.
- Tatu, wananchi ndio wana uwezo ya kutoa kiwango ya mishahara ya wabunge na rais na pia Councillors. Rais

asiwe na mamlaka zaidi, yaani above the law.

- Katiba ifundishwe shule kama subject zingine. Wabunge wachungunzwe kila baada ya miaka miwili na nusu, ikiwa hawajatumikia wananchi, waondolewe na wananchi wachaguane tena.
- Hakuna hukumu ya kifo ibadilishwe na iwe kifo cha maisha.
- Watoto wapate elimu ya bure.
- Kuwe na matibabu ya bure.
- Rais akistaafu, asijihusishe na siasa tena.
- Serikali iwe ikiundwa na vyama vyote vinavyo wakilishwa bungeni.
- Vitabu vya Katiba vipatikane kwa urahisi na kwa bei nafuu.
- Wakulima wakubaliwe kuuza mazao yao hata soko ya nje.
- Kodi inayotoshwa inputs za kilimo ipunguzwe ili mkulima apate faida. Example fertilizer inayouzwa Uganda inashuka Kenya, lakini ikifika Uganda, inauzwa kwa bei ya chini hapa nchini.
- Sheria inayoruhusu polisi kushika watu eti ni saa mbaya...

Com. Salome Muigai: Asante sana Bwana Joseph Kariuki Maina na asante kwa mfano wako mzuri. Amesema mambo kumi na magambi, karibu kumi na matatu kwa dakika mbili unusu. Fifteen, ametuambia mambo kumi na tano kwa dakika mbili unusu. Kwa sababu amekua focused kwa ile mapendekezo yake, tufuate hiyo mfano na tutaweza kusikiza watu wengi zaidi. Jackson Ngatia?

Jackson Ngatia: My name is Jackson Ngatia na mimi ni mkulima hapa Tabuga, niko na mambo mawili matatu ningetaka kutaja, ya kwanza ni education policy. Katika system ya siku hizi, kuna system ambayo ilikua introduced juzi juzi ya quarter system. Quarter system inawacha watoto ambao wamefanya vizuri zaidi, wanapakia nje, na wale wamefanya vibaya kutoka areas zingine, wanakua admitted katika high institutions. The entry zone mpaka university, mpaka mwisho wa Head office education institutions, ni kwamba huyo mtu atakua half baked. Ikiwa ni daktari utakuta ni a poor doctor, ikiwa ni another profession, atakua mtu ambaye ni poor. Na wote watakua katika market. Hiyo imeleta retardation kubwa katika maendeleo ya nchi yetu.

Kitu kingine ningetaka kusema kama mkulima ni kwamba small scale farmer ameteseka zaidi. Ndiye producer with particular emphases on horticultural farmer, iko kitu ambayo kilikua kinaitwa, Lommy convention. Katika Lommy convention, ilikuwa agreement ya kuuza vitu vyetu katika nchi za ng'ambo na European union. Hiyo ni mambo ambayo ingesemwa na mwananchi wa kawaida, lakini inapata only a privileged few, ambao wanakuza hizo vitu, wanauza for their own benefits.

Kwa hivyo ningetaka Ministry of Agriculture, particularly Co-operatives, ifanye kazi zaidi, ishike yule mkulima wa kawaida, small scale farmer ndiyo aweze kufaidika halafu ndio tumalize mambo ya umaskini katika hii nchi yetu.

Kitu nyingine Madam Commissioner na Commissioners, ningetaka kusema ni powers of the Presidency. Ni kwamba katika

kila jambo, unakuta ya kwamba the Heads ama Permanent Secretaries, Heads of Parastatal ndio wanakua appointed na Executive. Na wanakua controlled na yeye. Kwa hivyo hakuna kitu ambacho kinaweza kuenda mbele bila interference ya Executive. Niko na hayo tu, Commissioners. Thank you.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Stephen Njenga Kihanya? Did you appear before us yesterday?

Stephen Njenga Kihanya: Ya, very briefly,

Com. Salome Muigai: Yes, then I would like to give other people the chances before I give you a second chance.

Stephen Njenga Kihanya: It's okay Ms. Chair, I am going for a lecture at university of Nairobi at around five. So I will be very brief, two minutes.

Com. Salome Muigai: That I appreciate, as you can hear the people you want to represent, they want you to hear what they need, so please I am going to ask you to give this chance to somebody else, and then I will give you a chance after they have spoken. Stephen Njoroge Gicharu?

Stephen Njoroge Gicharu: My name is Stephen Gicharu from Nyanjoro farm. This are my comments.

- The President should not be above the law.
- His office should be taken to court when found guilty.
- The three arms of the government should have equal powers.
- Traditional drinks should be legalized, such as muratina, changaa, because they are African drinks, they should be packed by the government, examined and sold.
- Police should follow the law and not orders.
- The Constitutional book should be made available to everybody and printed in all Kenyan languages and made simple.
- The government should provide medical, water, electricity and primary education from the taxes it collects from the citizens.
- Elected MPs after being elected and found doing nothing should be elected out by the members. Thank you.

Com. Salome Muigai: Thank you, please register yourself. Christopher Mwangi?

Christopher Mwangi: Majina yangu ni Christopher Mwangi, na mimi ni mwenyeji wa hapa. Yangu ni machache sana. Kwanza ningeonelea Rais asiwe na nguvu ya kuchagua wakubwa wa police, Commissioner wa Police, Commissioner wa magereza. Kuwe na bodies, ziwe bodies zimekua formed, zitakua zikichagua wale wakuu wote wa serikali. Isiwe ni jukumu ya rais.

Pili, kuwe na either wakulima wawe wakipewa mikopo ya kuwezesha wao kulima kisha wawe wakilipa serikali hizo pesa baada ya kuuza mazao yao kwa serikali.

Tatu, katika elimu kuwe na njia ya kusomesha watoto wa primary kufikia mpaka standard eight, bila malipo, sababu hapo ndio inaoneka kuna kuwa na shida sana, ndio shinani ya kila kitu.

Kuwe na Commissioners wawe wakiangalia hali ya mishahara na mambo ya wabunge wenyewe. Wasiwe wakijikatia hali yao ya kibinafsi kwao wenyewe. Kuwe na board ya kuchunguza mishahara yao, maslahi yao, badala ya wao wenyewe ndio wanakata sheria huko na ndio wanajikatia. Ndipo wanajifanya kuwa na mishahara kubwa sana na mambo yao inakuwa zaidi sana.

Kusiwe na kukiwa ni budget ya mwaka huo, vile mambo nyingine ya mini-budgets, inasumbua, tunakuta kitu kimeongezwa na budget leo, baada ya wiki mbili, kuna vitu vingine pia vimeongezwa.

Katiba hii iweze kuandikwa na lugha ya kueleweka kama vile Kiswahili inavijitabu hizo, ziwe zikipelekwa ama ziuzwe kwa bei isio ya juu sana. Nafikiri ni hayo.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Timothy Nduhiu Kimathi?

Timothy N.Kimathi: Asante sana. Jina langu ni Timothy Nduhiu Kimathi naishi hapa hapa Tabuga. Yale niliyokuwa nayo ni haya. Mimi ni retiree nilikua nikifanya na Ministry of Agriculture.

Kwanza ningetaka serikali iangalie sehemu hii ya wakulima ambapo kuna importation ya agricultural products kama milk, sugar na the rest. Hiyo iangaliwe sana kwa sababu hakuna haja ya kuleta maziwa ama sukari kutoka nje, wakati viwanda vyetu vime lala tupu, kwa hivyo ingetakikana serikali iangalie sehemu hiyo.

Sehemu nyingine ni taxes za essential commodities za mwananchi wa kawaida, ziwe evaded, wasiwe wana tax mwananchi kwa sukari, sabuni, vitu ambavyo mwananchi anahitaji. Sehemu hiyo nyingine ni jua kali na agricultural tools, ama products za agriculture, production inputs za agriculture, taxes ziondolewe. Sababu hiyo ni sehemu muhimu sana kwa uchumi wetu. MPs nao, wanatakikana isiwe tu ni kazi ya mobilize wananchi kwa politics, waangalie pia wakiwafundisha watu sehemu ya AIDS, food security, education na other government policies.

President naye angalie, awe ni mtu ambaye ameelemika upande wa economics, awe pengine na diploma ama degree ya economics. Awe pia ni mcha Mungu.

Sehemu nyingine ni upande wa free education. Serikali iangalie kama imesema free education, iwe free kweli. Wa provide na kujenga mashule na pia kupeana vitabu, kuangalia sehemu ya watoto ambao hawajiwezi.

Pia kuwe na public security Commission, sababu kumekua na sehemu ya watu kulala nje kuangalia mali yao. Natural resources

Commission pia, iwe established sababu, umaskini mwingi umetokana na uharibifu wa misitu. Kwa hivyo tuangalie pia sehemu hiyo, ili misitu yetu ilindwe, bila misitu hakuna chakula. Kwa hivyo nilikua na hayo tu. Asante Bwana Commissioner.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Francis Muchiri?

Francis Muchiri: Commissioners, ladies and gentlemen, my name is Francis Muchiri and I am from Tabuga. I would like to make one or two observations because most of the things have been mentioned and I don't want to repeat. One of these is economic crime.

Kenya has been spoilt by a few people. It has been ruined because, the things that could have benefited many people in the country maybe goes to the pocket of an individual and then the rest of the masses do not get any benefit from that. So what I think is that we could curb this by introducing in the Constitution a very serious law on that, although many people are proposing that there should not be death penalties, I think this should be introduced in that one because, that will come as a crime. Anybody who has been involved in such kind of crime should not hold any public office and should be jailed for a long time as an alternative to death penalty.

I would suggest maybe fifteen to twenty years in jail. The other thing is about the retiring President. For the first time we are going to have a retiring President, I hope and we won't like a retired President to be involved in politics. Let him go and retire and enough is enough. Should he be involved in active politics, then all the benefits that accrue should be set aside. Be it transport, security or salary or whatever. He should not be given.

There should be a law that could be improved is the law of subjudice. You find some people to be so clever and take cases in court, and last for four, five or ten years and maybe they are of public importance. For example, the Goldenberg, people wanted to know who stole money and this kind of thing, but you see, these things drugged and nothing is happening. We do not seem to be getting anywhere. So could there be a limit, for such cases where the public has interest in such matters, so that they could be concluded within a given period. That is all.

Com. Salome Muigai: Thank you very much, please make sure that you are registered and now I would like to call, ningetaka kumwita Elizabeth Muthoni? Joan Wanjiru, Elizabeth Muthoni? Sio yeye, ni Elizabeth Muthoni, kuna list nyingine uliniletea mbele. Elizabeth Muthoni ni wewe mama? Oh na Joan Wanjiru? Okay, karibu.

Joan Wanjiru: Jina langu ni Joan Wanjiru, na nimeshukuru hawa wamekuja kwa haya maneno ya Katiba, maana sisi ni kama mara ya kwanza kukutana na mambo kama haya. Na sasa ninazungumza maneno ya wabunge. Habari ya miaka. Kama watu wako huko kwa bunge, tuseme ni kama vikundi vitatu, kuna vijana wa miaka kama thirty five, kuna watu wengine wa katikati wa miaka kama kutoka thirty five mpaka sixty hivi, kuna wengine wana miaka zaidi. Swali ni hili, hawa watu wako huko kwa bunge, mtu anachaguliwa mara ya kwanza, tena ya pili, hakuna limit ambaye mtu akifika mara fulani ndio atapumzika maana sisi

kama raia bado sikia, hiyo ni moja.

Tunaona hivi, ni vizuri kuangalia hiyo habari ya miaka zaidi, hatuwezi kusema maneno yote yako kwa bunge, ya Katiba ya mbeleni ni mbaya, maana kuna maneno mengine tunaona ya kwamba inaendelea vizuri.

Com. Salome Muigai: Mama Wanjiru ungependekeza lipi juu ya hii, wakati wa MPs ungependekeza nini?

Joan Wanjiru: Mtu anaweza kuchaguliwa kama mara mbili na ikizidi mara tatu, lakini mara ya tatu atakuwa amechoka, maana ni kazi ngumu. Sasa tunaona hivi, kama tuseme ni bibi ya President, tunaweza kuchagua mtu na ashindwe na mwenendo, maana sisi tunakaa hapa Kenya, na tukikaa hapa Kenya, tunakaa bila kupigwa na makabila mengine. Maana tuseme tunafanya urafiki na nchi nyingine, countries nyingine wanatusaidia kwa njia ya urafiki. Tukipata mtu awe wakati mwingine ashindwe na kuendelea hivi, awe ni wa hapa Kenya na anashindwa na mambo mengine, tunaweza kwenda mbaya, kwa hivyo ndio tunasema ya kwamba, tufikirie sana iletuko nayo na mambo yote ni sawa.

Tukitoka hapo ni maneno nyingine tulikua nayo ni maneno ya walimu. Walimu wana kazi nzuri na wameshafanya kazi yao, tukapata watoto wetu wameelimika na wamepata elimu, lakini kuna pahali moja tunaona kuna walimu wanataka kushikiliwa zaidi, walimu kama wa nursery school, wajie mpango wao ni nini. Nursery school wasiwe pamoja, hawa government wajaribu kutengeneza habari ya nursery school. Tunaona kama wao hawana mpango mzuri. Kama ni primary school ni sawa, kama ni secondary school ni sawa. Lakini wa nursery iko kitu inabakia.

Habari ingine ni hii, wa mama wa hapa Kenya, wapewe barua ya harusi. Maana tunaona hii wakina mama wameendelea sana, wanatumiwa na ma bwana, na hakuna sheria inasimamia wapatiwe harusi, kama tunaona hapa kwetu Kenya, lazima mtu yeyote apate kipande. Kama mtu ni bibi ya mtu, ni vizuri kupatiwa hiyo barua maana baadaye na tena anajulikana. Kwa hivyo barua inaonekana kama ni maneno muhimu.

Wakina mama wengine maechaguliwa kufika huko bunge. Swali iko hivi, akipata kura za kutosha anaweza kukubalika hapa kwetu Kenya kuwa President? Na maneno yangu ni hayo.

Com. Salome Muigai: Wewe mama ungetaka kupendekeza kitu gani juu ya wakina mama kuwa President.

Joan Wanjiku: Mama ninaona awe President, maana kuna wa mama wengine wanafanya kazi nzuri, na kuna wanaume wengine wanafanya kazi mbaya. Ikiwa kuna mama ambaye anaweza kufanya vizuri akipatiwa nafasi si vibaya.

Com. Salome Muigai: Asante sana kwa hayo maoni, jiandikishe pale tafadhali na sasa ninamwita Philip Maingi? Yuko. Kenneth Ndungu? Wewe ni Philip Maingi? Ulikuwa nje kidogo, okay, pole mzee. Philip tutakupa nafasi nyingine.

Philip Maingi: Jina langu ni Philip, na yangu ni machache, nina pointi karibu sita hivi. Ningependa kumaliza kumaliza ufasadi.

1. To end corruption, those who still from the government cofers, and have properties in their wives' names should have the property auctioned and repossessed by the government.
2. Dates for the general elections be made officical, hakuna haja ya President kukaa na hiyo date inakua ni kama dawa ya kuumiza wananchi. It should be at the end of four years or five years, tunapewa ni siku gani tunafanya elections, so that we are able kwenda ku-chage card zetu na kufanya inayotakikana.
3. Those found committing petty crimes, should not be locked in cells, but be given free bond to attend court the following day. This creates fear, ukiambiwa utawekwa cell, unaanza kuogopa na hapo ndio watu wanaanza kupeana pesa za kuhongana. Hiyo ikiondolewa, ukijua utapeleka kotini kesho, na umepewa free bond, itakua rahisi. Tena, kuwe na mtu ambaye amechaguliwa, someone to be selected to deal with cases that are delayed by advocates and those be given minimum time since some take a long time upto about ten to fifteen years. Na huyo mtu apeane, mwenye kutoa nafasi ya kusikiza hizo wakati, ajue ni kesi gani nzuri, asiwe delayed for a long time.
4. Reporters and final writers not to be arrested while on duty, their notebooks, cameras, video tapes zisiwe destroyed.
5. Mental patients to have counseling as soon as they leave hospital and have drugs free. Wasiwe wanauziwa madawa, kwa sababu ugonjwa wa akili ni ugonjwa ambayo inashika bila kujua. Ni hayo tu.

Com. Salome Muigai: Asante sana Mr. Maingi, jiandikishe tafadhali. Na sasa Kenneth Ndungu?

Kenneth Ndungu: My name is Kenneth Ndungu, ninataka ku bail kwanza na pointi ya retires, niliona pointi ya retirees ilikuwa drafted by my friend, Mr. Phaniel lakini kuna pointi ambaye aliacha inayohusika na adjustment. Mara nyingi tunaona wakati mishahara inakua revised, nothing is adjusted for the pensions, so ningetaka kupendekeza kuwa, wakati mishahara ya workers inakua adjusted, pia ya pensioners inakua adjusted accordingly. Inatakiwa kuwa adjusted tena kulingana na vile currency inabadilika. Kwa sababu from time to time, the value of the currency keeps on changing. So the salaries at the same time for the pensioners should be revised instead of being kept static.

Pointi nyingine, education in the country should be compulsory and free from nursery upto standard eight. University education should also be free. I recommend that part of the free fee for university should be in only the government universities and not every university, because those who go to private universities are the ones that are able.

I will recommend that the government should educate the first four children in a certain family. That is for an individual children, they should cater for four children and not every child so as to encourage family planning.

Kwa watoto wa mapipa, au the children that we call street children, I recommend that we have children departments which should be dealing with children. It used to be there before during the colonial time, I don't know where it went, if it were there we would not have any problem again.

Land policy, people should be allowed to own land anywhere in the Republic and nobody should be allowed to keep land that is idle. Any body who is not able to use his large s....of land, that land should be acquired by the government and be given to landless people. This landless people should not be given that land free of charge. It should be given as a kind of loan so that when they work on that land, what the profit they get, they pay something to repay to the government and return what the government used in acquiring that land from the owners.

Com. Salome Muigai: The last point?

Kenneth Ndungu: Last point I would like to touch something on the law. The law for compensation, you find that the compensation for injuries if one has had an accident, injuries compared to the compensation for defamatory are paid very little indeed. While defamatory is paid millions and millions of shillings. And in defamatory no one is hurt anywhere on the body, which speak of character being assassinated but nothing is touched on the body, while the person who is injured is actually maimed or moved on a wheelchair or something else and the compensation is too little compared to what we find being paid to defamatory. That is all, because time is gone. Thank you very much.

Com. Salome Muigai: Asante sana. Elizabeth Mwangi?

Elizabeth Mwangi: Thank you madam and the other Commissioners, I have quite a number of points here.

1. We should have a limited number of political parties in our country, not just so many parties because it is a multi-party state, we find that some of them will even belong to family, so can we have a limited number, maybe like two or three parties, so that the people in the country belong to either one or the other.
2. The Presidential powers also should be cut down and the President, I suggest should be elected by at least 50% of the population.
3. I also suggest that there should be some reservations of Parliamentary and civic seats for women and the youth, so that our women can participate fully in the government.
4. I also suggest that non-citizen should not be allowed to own land in our country.
5. The election date should be allowed in good time so that the candidates and the voters prepare themselves. It should not only be known to one person.
6. When it comes to salaries for workers, sometimes we find that the government appoints Commissioners to look into the salaries of certain groups, but even after they are given results by the Commissioners, they don't follow these results and yet so much money is used to keep the Commission going. So we want a government that will implement the findings of a Commission that it has appointed. For example we have the teachers' salaries, the Commissioners gave their findings and the government signed, they agreed, but they have not implemented that. In the Constitution this should be put down that we don't want a government that will cheat its' people.

